# HALMASHAURI YA WILAYA YA BUHIGWE

SHULE YA SEKONDARI MKOZA,
S.L.P 299,
BUHIGWE.
13. 12. 2020

**Kumb. Na. MSS/OR- TAMISEMI/ 1/ 2020**
Ndugu, ______________________________________________

______________________________________________

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MKOZA ILIYOPO WILAYA YA BUHIGWE KIGOMA.**

Nafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha KWANZA katika shule ya Sekondari Mkoza mwaka 2021. Shule hii ipo kijiji cha Kinazi kata ya Kinazi wilaya ya Buhigwe takribani kilometa 32 kutoka makao makuu ya wilaya ya Buhigwe.

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA NI KAMA YAFUATAYO**

1. Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021, hivyo unapaswa kuripoti shuleni siku ya tarehe hiyo kwa ajili ya kuanza masomo rasmi.
2. Mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe 24/01/2021. Hivyo jali muda uliopangwa kwani baada ya hapo taratibu za kisheria zitafuata kwa wanafunzi ambao hawataripoti.

**SARE ZA SHULE**

✓ **Wavulana**:

1. Suruali mbili rangi dark bluu ziwe na rinda mbili huvaliwa kwa muda wamasomo tu. Mshono wa suruali usiwe wa modo au mshono wa jinzi.
2. Suruali mbili rangi nyeusi ziwe na rinda mbili huvaliwa kwa muda wamichezo
3. Shati mbili nyeupe mikono mifupi
4. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba (gidamu) na kisigino kifupi. Viatu visiwe raba au tafu buti.
5. Soksi nyeusi jozi mbili au zaidi.

✓ **Wasichana:**

1. Sketi mbili dark bluu ziwe za mshono wa rinda box huvaliwa kwa muda wamasomo tu na kitambaa chake kiwe kama cha wavulana yaani kizito (*isiwe sukariksukari)*.
2. Urefu wa sketi ufunike magoti hadi juu kidogo ya fundo za miguu. Yaani kuacha sentimita 25 kutoka aridhini (chini).
3. Sketi mbili zambarau ziwe zenye rinda zisizozidi 16 huvaliwa kwa muda wamichezo na kitambaa chake kiwe cha *sukariksukari kwa vipimo vilivyotajwa hapo juu namba 2.*
4. Shati mbili nyeupe mikono mifupi na kwa wanafunzi wa kiislamu mikono mirefu na hijabu nyeupe yenye kufunika mwili mzima kama maelekezo yao yanavyosema.
5. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba (gidamu) na kisigino kifupi. Viatu visiwe vya aina ya raba, nta (bajaji) au tafu buti.
6. Soksi nyeupe jozi mbili au zaidi.

**NB**: 1. Tisheti kwa wanafunzi wote ni rangi ya chenza nzito yenye kola. (isiwe babalance).
2. Wanafunzi wote waripoti wakiwa na vivuli vya vyeti vya kuzaliwa.

Hongera kwa kuchaguliwa kujiunga kidato cha kwanza.
Karibu sana shuleni.

…………………………

**PILOT M. KISANGANYA**
**KAIMU MKUU WA SHULE**
**0626237225**

For The HEAD MASTER, P.O.Box 299 BUHIGWE DATE 13/12/2020 … SCHOOL

# SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

*(Tafadhari soma kwa makini sheria na kanuni za shule)*

**NIMARUFUKU**

1. Kuiba au kujihusisha na wizi wa aina yoyote
2. Kujihusisha au kufanya uesharati, ubakaji au ushoga
3. Kutumia pombe, madawa ya kulevya au kwenda bar
4. Kuvuta sigara, mirungi na bangi
5. Kupata au kutoa mimba au kusababisha mimba
6. Kuoa au kuolewa
7. Kupigana au kupiga
8. Kuharibu kwa kusudi mali ya umma
9. Kudharau bendera ya taifa au picha za viongozi
10. Kutoroka vipindi vya darasani, michezo au shughuri zozote za nje
11. Kugoma, kuchochea migomo au kuongoza migomo au kuvuruga amani na usalama wa watu.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi
13. Kusema uongo, kudhihaki na kurusha mikono, maneno kwa walezi au watu wengine
14. Kukwepa au kutegea kazi za mikono, mazoezi, majaribio ya mitihani ya ndani, wilaya, mkoa, kanda au taifa kwa ujumla.
15. Kuvaa sare bila nidhamu au bila kufuata taratibu za uvaaji wa sare mfano suruali au sketi kutokuwa na kisikizo au zipu, kuvaa suruali bila mkanda au kuvaa viatu bila soksi za shule.

    Au

    Kutepetesha suruali au sketi, kutochomekea shati au fulana, kukunja suruali au mikono ya shati au kuvaa sare za shule kama aina yoyote ya mtindo wa kihuni.
16. Kuvaa heleni, mikufu, bangiri, rozali au kipuli puani na vingine vya namna hiyo.
17. Kufuga nywele au ndevu, kutinda nyusi, kunyoa kipara, panki au viduku au mitindo ya aina yoyote kama fasheni
18. Kupaka wanja, shedo au poda au superblack au kujipodoa kwa aina yoyote ile mfano kwa kujichubua kwa vipodozi vya aina yoyote.
19. Mwanafunzi haruhusiwi kuwa au kumiliki simu ya mkononi, hivyo ikikamatwa haitarudishwa daima.

**KIAPO CHA MWANAFUNZI**

Mimi…………………………………………………………………………….(*taja majina yako matatu*) nimezisoma na kuzielewa sheria na kanuni zote za shule kwa usahihi na nikienenda kinyume na sheria na kanuni hizo basi adhabu kali za kinidhamu zichukue mkondo wake ikiwa ni pamoja kusimamishwa masomo au hata kufukuzwa shule kabisa.

**MAONI YA MKUU WA SHULE**

Nakutakia maandalizi mema na karibu sana mkoza sekondari

Motto wa shule "*Quality and Equal Education for All*"

____________________________

PILOT M. KISANGANYA

KAIMU MKUU WA SHULE

For The HEAD MASTER, P.O.Box 299 BUHIGWE DATE 13/12/2020 MKOZA SECONDARY SCHOOL

For the HEAD MASTER
P.O.Box 299
BUHIGWE
DATE 13/12/2020
MKOZA SECONDARY SCHOOL

# MKOZA SECONDARY SCHOOL

## FORM C

## MEDICAL EXAMINATION

(To be completed by a medical Officer in respect of all for I)

Entrance pupil's full name ..........................................................................
Age ........................................ (Years) Sex .............................
Blood count (Red and White) ...................................................................
Urinalysis.................................................................................................
Syphilis Test ............................................................................................
T.B Test ....................................................................................................
Eye Test ...................................................................................................
Chest ........................................................................................................
Spleen .......................................................................................................
Additional information: E.g Physical defects of Impairment(s)
Chronic infection or family disease.

I certify that I have examined above pupil and recommend that he/she is fit/unfit o pursue further Education.

Signed ..............................................................

Designation ......................................................

**(OFFICIAL STAMP)**

Date ______________________________

Delete whichever is inapplicable.